Imefadhiliwa na:

TOOLKIT COK-01: Jinsi ya kukusanya, kuandaa na kuhifadhi mbegu, na kuchagua eneo la kupanda kitalu cha *Ocimum kilimandscharicum*

1

Kusanya mashina ya mbegu yaliyokomaa kutoka kwa mimea wakati usio wa mvua, upepo, au matope.

2

Kata mashina ya mbegu kutoka kwa mimea ukitumia mikono au jozi ya makasi na kuweka vipandikizi ndani ya kikapu, mfuko au ndoo.

3

Kausha mashina ya mbegu nje kwenye mkeka chini ya kivuli kwa siku 2 hadi 3.

4

Baada ya kukausha mashina, pura ili kuondoa taka na kuacha mbegu pekee. Hii ni kwa sababu taka zikipandwa pamoja na mbegu, huelekea kuoza na kuhamasisha magonjwa ya fangasi.

5

Peta mbegu kwa kupiga mbali maganda na taka nyingine ya mimea (makapi) kwa kumwaga mbegu kutoka chombo kimoja hadi kingine au kutikisa na kupiga katika bakuli.

Washirika:

Imefadhiliwa na:

6

Mbegu ya *Ocimum kilimandscharicum* ni nyeusi na ndogo sana, yenye umbo la mviringo.

7

Hifadhi mbegu ikiwezekana katika makopo au katika mifuko ya karatasi kwenye pahali baridi, pakavu. Usihifadhi mbegu katika mifuko ya nailoni. Kama mbegu ikipata unyevu au joto, zinaweza kushindwa kuota.

8

Chagua eneo mzuri kwa ajili ya kuanzisha kitalu. Eneo lazima liwe tambarare, na lisiwe mbali na maji na pia nyumba. Ni lazima eneo liwe na udongo ambayo itaruhusu maji kuingia chini.

9

Eneo lazima liwe na ua ili kuzuia mifugo isiingie, na pia miti chache ili kutumika kama kinga dhidi ya upepo, lakini si kwa kivuli na miti minene.

Washirika:

Kwa habari zaidi, wasiliana na Bioprospecting Programme, *icipe*. Sanduku la posta 30772 - 00100, Nairobi. Email: icipe@icipe.org | www.icipe.org